Serikali ya Awamu ya Tano

Akiomba kura kwa wanan-

wa hadhara katika uwanja wa Kalangalala mjini humo,

watumishi 192 wamepelekwa katika Mkoa wa Geita.



MWANANCHI UK 11

# Serikali ya CCM kununua meli tano za uvuvi ukanda wa pwani

Mwandishi wetu, Nakungurukuru, Lindi

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali imepanga kununua meli tano kubwa za uvuvi zitakazotumika katika ukanda wa pwani, lengo likiwa ni kutoa fursa zaidi ya ajira kwa vijana na kuwawezesha Watanzania kunufaika na rasilimali za bahari katika ukanda huo.

Ununuzi wa meli hizo utakwenda sambamba na ujenzi wa bandari ya uvuvi ambayo meli zote zitakazovua kwenye eneo la bahari ya Tanzania zitatakiwa kutia nanga ili kuwe na mapato stahiki ya Serikali.

Akizungumza na wananchi wa Nangulukulu, Mkoa wa Lindi wakati akiwa njiani kuelekea Mtwara, Mhe. Samia amesema hatua hiyo itasaidia kuondoa wizi uliokuwa ukifanywa na meli za uvuvi zinazovua samaki ukanda wa bahari ya Tanzania.

"Tutanunua meli tano za uvuvi ambazo tutawafundisha vijana wetu kuvua samaki katika eneo letu la bahari, pia tutajenga bandari ya uvuvi ambayo meli zote za uvuvi zitatia nanga na tutafahamu kiwango cha samaki walichovua ili tupate mapato yetu badala ya kuibiwa," ameeleza Mgombea Mwenza.

Aliwaomba wakazi hao kumchagua Dkt. John Pombe Magufuli ili kukamilisha mambo yote hayo yanayolenga kujenga uchumi wa watu wa mikoa ya kanda ya Kusini.

"Chama pekee kilichojipanga kuwaletea Watanzania maendeleo ni CCM. Tutaleta maendeleo kwa vizazi vya leo na vinavyokuja," Mama Samia amebainisha.

Aidha, akizungumza na wananchi wa Mchinga, Mhe. Samia amewaeleza kuwa Serikali inatambua changamoto ya maji katika eneo hilo na kwamba baada ya miaka miwili ijayo shida ya maji katika eneo hilo itakuwa imetatuliwa.

Kuhusu shida ya kivuko kutoka Mchinga moja hadi Mchinga mbili, Mama Samia amesema atatuma wataalamu wa vivuko kuangalia eneo hilo ili changamoto hiyo iweze kutatuliwa.

Kwa upande wake Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete amesema wananchi wa Lindi wasubiri neema kutokana na ujio wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi Likong'o.

Amesema kiwanda hicho kitakuwa na thamani ya dola bilioni 30 ambapo pia mji wa kisasa utajengwa na wananchi kunufaikaikiwemo kupata ajira.

"Asiwadanganye mtu, maendeleo yanapatikana. Hakuna wa kubabaika wala kubabaishwa. CCM ni Chama chenye viongozi makini," alieleza.

Scanned with CamScanner

Mpigapicha Wetu)



MAJIRA UK 8.

# RC aanza msako watendaji waliowatoza fedha wafugaji

**Na Vincent Tiganya, Tabora**

WAFUGAJI mkoani Tabora waliotozwa tozo zisizohalali na kupewa stakabadhi zilizoandikwa kwa mkono wametakiwa kujitokeza na kuzileka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili wahusika wachukuliwe hatua kwa tuhuma za kuwaibia.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora Dkt. Philemon Sengati wakati wa mkutano kusikiliza kero mbalimbali za wafugaji kutoka Halmashauri zote.

Alisema Serikali ya Mkoa wa Tabora haiwezi kuendelea kukubali kuona wafugaji wanatozwa tozo zinazowaumiza na zinazotolewa kwa njia ya kificho na mara nyingi katika maeneo ya porini ambako hakuna mtandao wala Benki.

Mkuu huyo wa mkoa alisema tozo hizo na zile zinadaiwa kuwa zoto za meza zinatozwa na Watendaji wa Vijiji na Kata kama tozo ya Meza hizo zote ni rushwa ,lazima ikomeshwe.

Dkt.Sengati aliwaomba wafugaji wote ambao wameumizwa na tozo zisizo rasmi washirikiane na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa kutoa taarifa kwa ajili ya kuwatafuta na kuwakamata wahusika wote ili waweze kurejesha fedha za walizochukua.

Alisema kama wamefanikiwa kurejesha fedha za wakulima wa tumbaku ambao walikuwa wamedhulumiwa na viongozi wasio waaminifu hawawezi kushindwa kurejesha fedha za wafugaji.

Aidha Dkt. Sengati ameagiza misako yote dhidi ya mifugo ni lazima ipate kibali kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili kuzuia wafugaji kunyanyaswa.

Alisema lengo kutaka kuzuia tozo ambazo haziko katika utaratibu unaokubalika ili kuhakikisha mfugaji anaendesha shughuli zake kwa amani na utulivu bila kuvunja sheria.

Mfugaji kutoka Kipili ,Wilaya ya Sikonge Mwita Sumaku alisema ng'ombe wake 169 walikamatwa akatozwa shilingi milioni 5 , lakini stakabadhi aliyoandikiwa ilionyesha milioni 2.

Scanned with CamScanner



CHAGUA CCM

# Mabadiliko makubwa ya kisayansi katika ufugaji

Sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi. Kutokana na umuhimu huo, ni dhahiri kuwa ipo haja ya kuendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa na kuchakata/kusarifu bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani, ikiwemo ya lishe bora, na usafirishajinje. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020) Chama Cha Mapinduzi kilijielekeza katika kuhakikisha sekta ya ufugaji inaimarishwa ili kuwawezesha wananchi kunufaika na ukuaji wa sekta hiyo.

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na kuimarika kwa sekta ya ufugaji kwa kuongeza uhamilishaji wa ngiombe na uzalishaji wa mbegu bora za mifugo; kuongeza uzalishaji wa chanjo za mifugo ili kupunguza magonjwa yanayoenezwa na wadudu, maboresho ya sera, sheria na kanuni katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya mifugo na kuongeza maeneo ya malisho yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuimarisha mashamba matano ya kuzalisha mifugo ya Sao Hill, Mabuki, Ngerengere, Kitulo na Nangaramo pamoja na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) ambapo mitamba 51,735 ilizalishwa katika mashamba ya Serikali, NARCO na Sekta Binafsi na kusambazwa kwa wafugaji;

(b) Kuongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2015 hadi hekta milioni 5.0 mwaka 2020; ambapo hadi mwaka 2020 Vijiji 1,852 vimeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kati ya Vijiji 12,545 vilivyopo nchini ambapo maeneo ya malisho hekta 2,788,901.17 yametengwa kwa ajili ya ufugaji katika Mikoa 22;

(c) Kujenga na kukarabati mabwawa ya Nyakanga (Butiama) na Wami - Dakawa (Mvomero) na hivyo kufanya idadi ya mabwawa/malambo kufikia 1,482 mwaka 2020 kutoka 1,378 mwaka 2015 sawa na ongezeko la malambo 104;

(d) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ufugaji kiasi cha shilingi bilioni 22;

(e) Kuongeza idadi ya ngiombe waliohamilishwa kutoka 105,000, mwaka 2015 hadi 514,700, mwaka 2020. Mitungi 71 ya kuhifadhi kimiminika cha naitrojeni (lita 35) na vifaa vingine vya uhamilishaji na usafiri vimenunuliwa. Aidha, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 2.1 mwaka 2015 hadi lita bilioni 2.7 mwaka 2020;

(f) Kudhibiti magonjwa ya mifugo ambapo lita 21,373.06 za dawa za kuogeshea mifugo zilisambazwa katika Mikoa 25, Halmashauri 152 katika majosho 1,738 yanayofanya kazi. Aidha, majosho mapya 104 yamejengwa na 301 yamekarabatiwa;

(g) Kuboresha huduma za chanjo za magonjwa ya mlipuko yanayoathiri afya ya mifugo na binadamu na kuwezesha biashara ya mifugo katika soko la kimataifa, ambapo wastani wa upatikanaji wa chanjo umeogezeka kwa baadhi ya magonjwa na kupungua kwa mengine kutokana na uwepo au kutokuwepo kwa tishio la ugonjwa husika nchini kama ifuatavyo;

(i) Wastani wa upatikanaji wa chanjo ya mdondo wa kuku umeongezeka kutoka wastani wa dozi milioni 55 mwaka 2015 hadi dozi milioni 121 mwaka 2020;

(ii) Wastani wa upatikanaji chanjo ya ugonjwa wa Kimeta umeongezeka kutoka wastani wa dozi 500 mwaka 2015 hadi dozi 1,846,600 mwaka 2020;

(iii) Wastani wa upatikanaji chanjo ya ugonjwa wa kutupa mimba umeongezeka kufikia wastani wa dozi 3,825 mwaka 2020 tofauti na awali ambapo hakuna chanjo zilizotolewa;

(iv) Wastani wa upatikanaji chanjo ya ugonjwa wa chambavu umeongezeka kutoka wastani wa dozi 500 mwaka 2015 hadi dozi 2,045,870 mwaka 2020;

(v) Wastani wa upatikanaji chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa umeongezeka kutoka wastani wa dozi 122,550 mwaka 2015 hadi dozi 302,000 mwaka 2020; na

(vi) Kujenga kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha chanjo za mifugo aina 37 cha Hester Bioscience ñ Kibaha mkoa wa Pwani.

> Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na kuimarika kwa sekta ya ufugaji kwa kuongeza uhamilishaji wa ngiombe na uzalishaji wa mbegu bora za mifugo; kuongeza uzalishaji wa chanjo za mifugo ili kupunguza magonjwa yanayoenezwa na wadudu, maboresho ya sera, sheria na kanuni katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya mifugo na kuongeza maeneo ya malisho yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji.

(h) Kuongeza uzalishaji wa chanjo za mifugo katika kituo Kibaha (Tanzania Vaccine Institute-TVI) kutoka dozi 26,367,200 mwaka 2015 hadi dozi 185,867,275 mwaka 2020;

(i) Kuongeza udahili wa wanafunzi katika vituo 8 vya Serikali (LITA) kutoka wanafunzi 1,800 mwaka 2015 hadi wanafunzi 3,634 mwaka 2020;

(j) Kuongeza viwanda vya kusindika maziwa kutoka 82 mwaka 2015 hadi 99 mwaka 2020. Viwanda vya kusindika nyama nchini vimeongezeka kutoka 25 mwaka 2015 hadi viwanda 33 mwaka 2020. Aidha, kuna viwanda 9 vya ngozi ambavyo vimesaidia usindikaji wa ngozi wa hatua ya kati kufikia futi za mraba 124,420,000 kwa mwaka; na

(k) Kuongeza usindikaji wa maziwa kutoka wastani wa lita 167,620 mwaka 2015 hadi kufikia lita 194,335 kwa siku mwaka 2020.

Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitaelekeza Serikali kuendelea kuleta mabadiliko makubwa na ya kisayansi katika ufugaji kwa kuhimiza ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na utafiti wa mifugo ili kuzalisha ajira nyingi zaidi hasa kwa vijana na kuinua mchango wa sekta katika Pato la Taifa na kuleta ustawi wa wananchi. Aidha, Serikali itatakiwa kushughulikia kwa nguvu zaidi migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Ili kufikia azma hiyo, CCM itaelekeza Serikali kujikita katika kuboresha maeneo ya kimatokeo kama ifuatavyo:-

(a)Kuendeleza na kuimarisha huduma za Ugani katika ngazi za Kata na Vijiji kwa kuhakikisha kuwa kila mfugaji anafikiwa na huduma za Ugani na kwa wakati. Yafuatayo yatatekelezwa:-

(i) Kuongeza idadi ya maafisa ugani kwa kuajiri na kuhakikisha kuwa kila kata na kijiji kinafikiwa na afisa ugani au mtoa huduma za ugani nchini;

(ii) Kuimarisha usimamizi wa maafisa ugani, kuwawezesha na kuwapatia vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri na vifaa kazi vya uwandani ili kuwafikia walengwa;

(iii) Kuanzisha mashamba darasa na mashamba ya mfano ya malisho katika vijiji, halmashauri za wilaya na miji nchini;

(iv) Kuweka mkazo zaidi kwenye usambazaji wa teknolojia na kutoa mafunzo kwa wafugaji na wadau wote kwa njia ya machapisho, majarida, vipeperushi, vipindi vya redio na luninga;

(v) Kuongeza udahili kwa mwaka katika vyuo vya mafunzo ya mifugo nchini kutoka 3,634 mwaka 2020 kwa mwaka hadi 9,760 kwa mwaka 2025 ikiwa ni jitihada za kutosheleza mahitaji ya raslimaliwatu katika Sekta;

(vi) Kubuni na kutekeleza mipango ya kutoa mafunzo rejea kwa wafugaji na maafisa ugani katika halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi;

(vii) Kujenga mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha mashamba ya mifugo na jamii ya wafugaji wa asili kubadili namna ya kutekeleza shughuli zao za ufugaji na kuwa za kisasa;

(viii) Kutenga, kupima na kumilikisha maeneo ya shughuli za ufugaji kwa wafugaji katika halmashauri zote nchini;

(ix) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kwa kuboresha ranchi tano (Kongwa, Ruvu, Kalambo, Missenyi na West Kilimanjaro) ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo. Aidha, sekta binafsi na wafugaji mmoja mmoja watahimizwa kuendelea kumiliki na kuboresha miundombinu katika ranchi zao ili kuwa na ranchi za kisasa ndani ya Serikali na pia kwa wafugaji binafsi;

(x) Kuongeza na kuimarisha ujenzi wa machinjio ya kisasa katika maeneo yote nchini;

(xi) Kuimarisha utambuzi na usajili wa mifugo nchini ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wafugaji na mifugo yao;

(xii) Kuboresha maeneo ya wafugaji kwa kuyapatia huduma muhimu zikiwemo maji, afya na elimu kwa ajili kusaidia jamii hiyo kutulia sehemu moja na hivyo kuepuka kuhamahama kufuata huduma hizo; na

(xlii) Kuhamasisha jamii ya wafugaji wa asili na watumiaji wengine wa ardhi ili kuepuka migogoro ya kijamii kwa ajili ya kuhakikisha kuwa uchumi wa sekta ya ufugaji unafungamanishwa na uchumi wa sekta nyingine na kuchangia katika pato la Taifa.

(b) Kuendeleza na kuibua tafiti mbalimbali zenye kujibu changamoto za Sekta ya Mifugo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuibua na kufanya tafiti katika maeneo makuu ya vipaumbele vya maendeleo ya mifugo nchini. Aidha, tafiti 37 za muda mfupi na 26 za muda mrefu katika Agenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo zitafanyika; na

(ii) Kuendeleza taasisi za kitafiti ili kufanya tafiti ambazo zitajikita kutoa suluhisho kwa changamoto katika sekta ya mifugo ili kuongeza ubora wa mazao ya mifugo ikiwa ni pamoja na wingi wa nyama na maziwa; na ubora wa ngozi.

(c) Kuboresha afya ya mifugo nchini kwa kuimarisha kinga, chanjo na tiba kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa mifugo yote nchini inapatiwa chanjo kwa kuzingatia mpango na ratiba ya chanjo;

(ii) Kutoa chanjo za ruzuku kwa magonjwa 13 ya kipaumbele ili kuimarisha afya ya mifugo na binadamu nchini kwa kushirikisha sekta binafsi;

(iii) Kuimarisha upatikanaji wa chanjo na dawa za mifugo nchini kwa kujenga viwanda vya kuzalisha chanjo na dawa ili kutosheleza mahitaji;

(iv) Kuhakikisha kuwa kila halmashauri nchini inakuwa na mfumo baridi (cold chain) kwa ajili ya kutunza chanjo za mifugo;

(v) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa chanjo na kudhibiti kuenea kwa vimelea vya magonjwa kwa mifugo ili kuwa na mifugo yenye afya bora;

ITAENDELEA UHURU KESHO.



Scanned with CamScanner